

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAIRI ZA MAGARI, PIKIPIKI NA BAISKELI AMBAZO ZILISHATUMIKA

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 3 ya mwaka 1975 na kuanza kazi rasmi tarehe 16 Aprili 1976, kisha kuundwa upya kwa Sheria Na. 2 ya mwaka 2009 iliyoifuta sheria ya kwanza. Sheria mpya imelipa Shirika uwezo mkubwa zaidi wa kusimamia shughuli za utayarishaji wa viwango na udhibiti wa ubora.

TBS inapenda kuwakumbusha wauzaji, wasambazaji na watumiaji wa tairi za magari, pikipiki na baiskeli ambazo zilishatumika (used tires) kuwa haziruhusiwi tena kutumika. Basi iwapo itafanyika hivyo ni kinyume na matakwa ya Sheria Na. 2 ya mwaka 2009.

Tangazo hili litaenda sambamba na ukaguzi utakaofanyika kwenye soko kwa lengo la kubaini watakaokiuka agizo hili kwa kuendelea kufanya biashara ya kuuza au kusambaza tairi ambazo zilishatumika.

Limetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Viwango Tanzania,
S.L.P. 9524,
Dar es Salaam,
Simu: +255(022) 2450206
Hotline: +0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: www.tbs.go.tz